

## **Kanuni za kutohudhuria, ruhusa na likizo zinazohusu masomo ya lugha na kazi (Introduksjonsprogrammet)**

Kanuni za kutohudhuria masomoni ni sawasawa na zile kanuni za wafanyakazi. Tofauti moja tu ni kwamba huwezi kupewa ruhusa ya ugonjwa isiyo kamili. Kwa upande wa likizo ya kuruhusiwa zimetengenezwa kanuni za kujitegemea ambazo hazifanani na zile za wafanyakazi.

Ikiwa unaumwa ni lazima utoe taarifa kwa manispaa, mwalimu au kwa uongozi wa kule ulipoajiriwa kwa ajili ya mazoezi ya kazi. Wafahamisha kuwa hutaweza kuhudhuria. Ikiwa hutaweza kuhudhuria kwa sababu zinazokubalika, utakuwa na haki ya kulipwa mshahara wako kama kawaida. Ikiwa hutumii ruhusa ya kujipatia mwenyewe, wala huna ruhusa ya kutoka kwa tamko la daktari, au huna ruhusa maalumu, utapunguziwa mshahara wako kulingana na masaa ambayo hukuhudhuria, au siku zile ambazo hukuhudhuria. Hapo inahesabiwa kama vile umekuwa mtoro. Kutohudhuria masomoni bila sababu yaweza kuleta matokeo ya kufukuzwa shule na kukosa haki ya malipo ya mshahara.

### **Ugonjwa**

Likizo ya ugonjwa kwa kujipatia mwenyewe au kupatiwa na daktari yaweza kukubalika ikiwa umepatwa na maumivu ambayo yanakuzuia ushindwe kwenda masomoni. Ruhusa ya kujipatia mwenyewe utaitumia pale tu unapotoa taarifa kwa maandishi au kwa taarifa ya mdomo kwa manispaa, shule au mwalimu, au kwa mshauri wako, ya kwamba wewe ni mgonjwa.

- Unaweza tu kujipatia ruhusa ya ugonjwa pale ambapo umeshahudhuria atika masomo yako kwa majuma 8. Majuma 8 ya mwanzo waweza kutohudhuria kwa ruhusa kutoka kwa daktari tu ikiwa utakuwa mgonjwa.
- Unaweza kutumia ruhusa ya kujipatia mwenyewe wakati wa ugonjwa mara 4 tu katika kipindi cha miezi 12. Kila ruhusa ya aina hiyo waweza kuitumia siku tatu tu za kalenda.
- Ikiwa ugonjwa wako unaendelea zaidi ya siku 3 unapaswa kupata kibali cha daktari. Kanuni hii inatumika pia ikiwa umeshamaliza kutumia ruhusa zako mwenyewe mara 4 kwa miezi 12.

Ikiwa una mtoto mmoja au wawili, na imetokea kuwa mtoto ni mgonjwa, waweza kubakia nyumbani nao kwa muda wa siku 10 katika kipindi cha miezi 12.

Ikiwa una watoto zaidi ya wawili unaruhusiwa kubakia nyumbani na watoto wagonjwa kwa muda wa siku 15 katika kipindi cha miezi 12.

Ikiwa wewe ni mzazi peke yako, basi una haki ya kubakia nyumbani kwa siku 20 ikiwa una watoto wawili na ikiwa una watoto zaidi ya wawili, basi waweza kuruhusiwa siku 30.

Ikiwa una mtoto mwenye maradhi ya kudumu, au mlemavu, jambo ambalo linasababisha kutoweza kuhudhuria masomoni, basi una haki ya kubakia nyumbani kwa muda wa siku 20. Na ikiwa wewe ni mzazi peke yako, siku zinaongezeka hadi 40 katika kipindi cha miezi 12.

Mtu ambaye anakubalika kuwa ni mlezi peke yake aweza kuwa yule ambaye mwenzi wake yaani mume au mke amekuwa na matatizo ya kutoweza kulea watoto, labda kwa sababu ya ulemavu au kwa sababu ya ugonjwa wa muda mrefu unaosababisha alazwe katika taasisi zinazosaidia watu wa aina yake.

Haki hizi zinahusika pia ikiwa mwangalizi wa watoto (yaya) ni mgonjwa.

Ikiwa umeshindwa kuhudhuria kwa siku 3 mfululizo, manispaa yaweza kudai taarifa kutoka kwa daktari juu ya ugonjwa wa muangalizi wa watoto.

## **Ruhusa ya kutohuduria masomoni**

### *Likizo kutokana na ujauzito (mimba)*

Ikiwa wewe ni mjamzito una haki ya kutokuhudhuria masomoni bila kukatwa mshahara wako unapokwenda kwa mganga kwa ajili ya uangalizi wa maendeleo ya mimba ikiwa hakuna muda muafaka nje ya saa za masomo. Wakati wa ujauzito, unaruhusiwa kutohudhuria masomoni kwa kwa siku 10 bil kuathiri mshahara wako.

### *Ruhusa ya kunyonyesha*

Ikiwa mtoto wako ananyonya, unaruhusiwa kila siku ya masomo kutumia saa 1 ya kunyonyesha hadi mtoto atakapotimiza mwaka mmoja.

## **Kibali cha kujifungua au cha kupata mtoto wa kupanga kitolewacho bila mshahara**

Wazazi wanaohudhuria katika masomo wana haki ya ruhusa ya kumtunza mtoto anapozaliwa hadi atimize miezi 10 ya mwaka wa kwanza wa mtoto.

Manispaa itakaribisha uwezekano wa kufuatilia, kufundisha elimu ya lugha na mazoezi ya lugha ikiwa una likizo ya mzazi au umepata mtoto wa kupanga. Mpango huu utatolewa na manispaa hadi mwezi wa nne wa kibali chako cha muda wa ruhusa kama vile wewe unavyotaka.

Ikiwa imetokea kwamba wazazi wanaohudhuria masomoni wamepata mtoto wa kupanga ambaye umri wake hauzidi miaka 15, basi wanaruhusiwa kubakia nyumbani na mtoto huyo hadi miezi 10.

Ikiwa wazazi wote wawili wa mtoto wa kupanga wanakwenda masomoni, basi siku 75 za ruhusa zitakuwa kwa ajili ya baba na siku 75 kwa ajili ya mama. Baba asipotaka kutumia haki yake ya likizo, basi inakuwa imekwisha hivyo. Katika hali isiyo ya kawaida, kanuni hii yaweza kutumika kwa namna nyingine, kwamba ile likizo ya baba yaweza kutumiwa na mama ikiwa baba ni mgonjwa, ama ameumia kiasi kwamba anahitaji msaada wa kumtunza mtoto wake, au ikiwa amelazwa katika taasisi ya afya. Hali kama hii sharti iwe na taarifa za kitabibu kutoka kwa mganga.

## **Ruhusa za aina mbalimbali**

Waweza kuiomba manisipaa yako ikupatie ruhusa maalumu ya kijamii ikiwa kwa mfano unapaswa kwenda kumuona daktari au mganga wa meno, katika usaili wa kazi, au jambo lingine. Waweza pia kuomba ruhusa ya kijamii pale ambapo mtoto wako anaenda kuanza shule, au chekechea (barnehage), au kama kuna msiba wa ndugu wa karibu yako na kadhalika. Waweza kupata maelezo zaidi kutoka kwa mshauri wako wa mipango ya masomoni.

Taarifa za kitabibu zinaweza kukupatia kibali cha kuruhusiwa kupata likizo ya mwaka mzima bila malipo ya mshahara ikiwa mtoto wako amepatwa na ugonjwa unaodumu kwa muda mrefu.

## **Sikukuu na siku maalumu**

Watu wote watakuwa na siku mbili za mapumziko kila juma yaani jumamosi na jumapili (Siku ya soko na siku ya mungu)

Siku zifuatazo ni sikukuu hapa Norway, hivyo zinatupatia ruhusa ya kutohudhuria masomoni bila kuathiri malipo ya mshahara: Tarehe 1 na 17 mwezi wa mei, Tarehe 1 ya mwaka mpya, Alhamisi ya majivu, Ijumaa kuu, Jumatatu ya pasaka, sikukuu ya kupaa kwa Yesu, Siku ya pili ya Pentekoste, na tarehe 25 na 26 za mwezi wa desemba baada ya noel (krisimasi)

Kama wewe una dini nyingine nje ya sikukuu hizi za kitaifa, basi una haki ya kuomba ruhusa ili uweze kuadhimisha sikukuu yako kwa siku mbili kila mwaka kulingana na matakwa ya dini yako bila kuathiri malipo ya mshahara wako. Ni sharti kwamba utoe taarifa ya sikukuu yako kwa manisipaa siku 14 kabla ya sikukuu unayotaka kutumia haki ya ruhusa yako kufika.

## **Likizo**

Una haki ya siku 25 za likizo kila mwaka. Manisipaa yako ina wajibu wa kuamua kwamba likizo yako iwe wakati gani. Una haki ya kulipwa mshahara wako wakati wa likizo yako.